| | |
|---|---|
| **Swahili**<br>**INFORMED CONSENT**<br>Women's Health Needs Study Informed Consent to be a Research Participant | **RUHUSA KWA KUJUA**<br>Ruhusa ili kuwa Mshiriki wa Utafiti wa Mahitaji ya Afya ya Wanawake |
| My name is _______________and I am working with NORC and the Centers for Disease Control and Prevention on this study. | Jina langu ni ________________ na ninafanya kazi na NORC na Senta za Kuthibiti na Kuzuia Magonjwa katika utafiti huu. |
| Why we are doing this study? We are trying to find out about the health care needs of women age 18 to 49 years in your community. We plan on interviewing about 100 women for this study. | Mbona tunafanya utafiti huu? Tunajaribu kujua kuhusu mahitaji ya huduma za matibabu ya wanawake kati ya miaka 18 hadi 49 katika jamii yako. Tunapanga kuhoji kadri ya wanawake 100 kwa utafiti huu. |
| Who is funding this study? This study is funded by the Centers for Disease Control and Prevention. | Je, ni nani anatoa rasilimali za utafiti huu? Utafiti huu unapata rasilimali kutoka kwa Senta za Kuthibiti na Kuzuia Magonjwa. |
| What would I be asked to do if I am in this study? | Je, ni nini nitaulizwa nifanye iwapo nipo kwenye utafiti huu? |
| The interview will take you about 45 minutes. | Mahojiano yatachukua kadri ya dakika 45. |
| We will read you the questions in your preferred language. | Tutasoma maswali yako katika lugha unayopendelea. |
| We will be asking you some questions to see if you are eligible to be in the study. | Tutakuwa tunakuuliza maswali kuona iwapo unafaa kuwa katika utafiti. |
| These will be about things like where you and your family are from, what languages you speak, and if you have lived in certain countries. | Haya yatakuwa kuhusu vitu kama vile familia yako inatoka wapi, lugha unazozungmza, na iwapo umeishi katika mataifa |
| If you are eligible, give consent, and then choose to enroll in the study, then we will be asking you questions such as how long you have been in the US, if you have had a medical exam, your childbirth experiences, and what you and your family thinks about female circumcision and your experiences with female circumcision. | Iwapo unafaa, peana ruhusa, kisha uchague kushiriki katika utafiti, halafu tutakuuliza maswali kama vile muda ambao umekuwa Marekani, iwapo umekuwa na uchunguzi wa kiafya, uzoefu wako kuhusu kujifungua, na ni nini wewe na familia yako inafikiria kuhusu tohara kwa wasichana na uzoefu wako na tohara kwa wasichana. |
| Some of the study questions may make you feel uncomfortable. You can skip any question. Your answers are completely private and only results from the whole group of women will be included in any report. | Baadhi ya maswali ya utafiti yanaweza kufanya uhisi kuwa una uzito. Unaweza ruka swali lolote Majbu yako ni ya siri na ni matokeo kutoka kwa kikundi kizima cha wanawake yatajumuishwa katika ripoti yoyote. |
| How long will it take for me to participate in this study? For this study you will do one interview that will take about 45 minutes to complete. This will end your time in the study. | Je, itanichukua muda upi ili kushiriki katika utafiti huu? Kwa utafiti huu utafanya mahojiano ambayo itachukua kadri ya dakika 45 ili kukamilisha. Hii itakamilisha wakati wako katika utafiti. |
| Are there any risks for me if I decide to participate? The risks to participating in this research are minimal. However, some of the questions are personal and might make you uncomfortable. You are free to skip or not answer any questions. You can stop at any time. I have community resources available for you if you | Je, kuna hatari yoyote iwapo nitaamua kushiriki? Hatari za kushiriki katika utafiti huu ni chache. Hata hivyo, baadhi ya maswali ni ya binafsi na yanaweza kufanya uwe na uzito. Una uhuru wa kuruka mawali yoyote. Unaweza kuacha wakati wowote. Nina rasilimali za jamii ambazo unaweza kutumia iwapo unahitaji usaidizi au huduma katika jamii yako. |

| | |
|---|---|
| need help finding support or services in your community. | |
| If you choose to do the survey whether you complete the survey or not, you will not lose access to any services that you would otherwise be eligible for. Your answers will be kept private to the extent allowed by law and will be used only for research. The study has a Certificate of Confidentiality, so no one outside the study, even an official of the court, the government or law, can request your information. However, if interviewers and other study staff learn of plans to have your minor daughter circumcised they may be legally obligated to report this as child abuse to state or local authorities The study does not ask you about circumcision in your daughter. | Iwapo utachagua kufanya utafiti, kama utakamilisha au la, hutapoteza ufikiv wa huduma zozote ambazo ungepata. Majibu yako yatawekwa kuwa ya siri hadi kadri ambayo inaruhusiwa na sheria na itatumiwa tu katika utafiti. Utafiti una Cheti cha Usiri, kwa hivyo hakuna ambaye yuko nje ya utafiti, hata afisa wa koti, serikali au sheria, anayeweza kuitisha habari zako. Hata hivyo, iwapo wahoji na wafanyakazi wengine wa utafiti watajua kuhusu mipango ya kumtahiri binti yako, watakuwa na wajibu wa kisheria kuripoti hili kama kumdhulumu mtoto kwa mamlaka ya nchi au mkoa. Utafiti hauulizi kuhusu kumtahiri binti yako. |
| Employees of CDC, or experts and contractors working for CDC, may review information sent through computer networks to assess security. We will not collect your name or other information that identifies you during this interview. When results from this research are presented, we will not include any information that might be used to figure out who you are. | Wafanyakazi wa CDC, au wataalamu na kontrakta wanaofanyia CDC kazi, wanaweza kuona habari ambazo zimetumwa kupitia mitandao ya tarakilishi ili kukadiri usalama. Hatutachukua jina lako au habari nyingine ambazo zinakutabulisha katika mahojiano haya. Wakati matokeo yatatolewa, hatutajumuisha habari zozote ambazo zinawezatumiwa |
| Are there any benefits for me if I decide to participate? There is no direct benefit to you for participating in the study. We believe the answers you provide will help us better understand the health care needs of women in your community. | Je, kuna manufaa yoyote iwapo nitaamua kushiriki? Hakuna manufaa yoyote yanayoonekana kwako unaposhiriki katika utafiti. Tunaaminai majibu utakayotoa yatatusaidia tuelewe mahitaji ya huduma za afya za wanawake katika jamii yako. |
| Payment for participation: If you agree to be in this study we will give you $20 for your travel and/or child care expenses. In addition, if you recruit another women to be in this study, we will give you $5 for cell phone calls and/or transportation. You may recruit up to 3 women and receive $5 for each woman you recruit. You may need to contact these 3 women with our study invitation card. You will be able to receive a total of $35 reimbursement for expenses you may need to participate in the study and for recruiting up to three women. | Malipo kwa kushiriki Iwapo utakubali kushiriki katika utafiti huu, tutakupa $20 kwa ajili ya kusafiri na/au gharama za kutunza mtoto wako. Vilevile, iwapo utasajili wanawake wengine kuwa katika utafiti huu, tutakupa $5 kwa kupiga simu na/au kusafiri. Unaweza kuita hadi wanawake 3 na utapokea $5 kwa kila mwanamke utakayesajili. Unawezahitaji kuwasiliana na wanawake hawa 3 kutumia kadi yetu ya mwaliko wa utafiti. Utaweza kupokea hadi $35 kwa gharama ambazo utapata ili uweze kushiriki katika utafiti na kwa kusajili hadi wanawake watatu. |
| A unique passcode will let us know which women you helped recruit so that we can reimburse you. Your name will not be collected at any time during this study. | Kuna kodi maalum ambayo utatujulisha ni wanawake wepi ambao ulitusaidia kusajili ili tukulipe. Jina lako halitachukuliwa wakati wowote katika utafiti huu. |
| Do I have to be in this study? No you do not. If you choose to be in this study, you can stop at any time and you are also free to skip or not answer any questions. | Je, ni lazima niwe katika utafiti huu? La si lazima Iwapo utachagua kuwa katika utafiti huu, unaweza wacha wakati wowote na pia jihisi huru kuruka na kutojibu maswali yoyote. |

What happens if I would like to stop this interview? If you start the interview and decide to stop, that is perfectly OK. You will still receive the $20 for your travel and/or any child care expenses you may have during this interview.

Ni nini itafanyika iwapo nitataka kuwacha utafiti huu? Iwapo utaanza na uamue kuwacha, hiyo ni sawa kabisa. Bado utapokea $20 kwa usafiri wako na gharama zozote za mtoto utakazopata wakati wa mahojiano haya.

We will be able to keep and use the information you have shared up until that point. If you do not want your responses to be included, let us know and we will destroy your information.

Tutaweza kuweka na kutumia habari ambayo umetoa hadi ulipowachia. Iwapo hungependa majibu yako yatumiwe, tujulishe na tutaharibu habari zako.

Right to Ask Questions: Please contact Field Coordinator at (XX) with questions, complaints or concerns about this research. If you have any questions or concerns about your rights as a research participant, please contact the NORC IRB Manager by toll-free phone number at (866) 309-0542. An Institutional Review Board (IRB) operates under Federal regulations and they review research involving human subjects to ensure the ethical, safe, and equitable treatment of study participants.

Uhuru wa Kuuliza Maswali Tafadhali wasiliana na mratibu wa kiwanja kupitia (XX) na maswali, malalamishi au shaka kuhusu utafiti huu. Iwapo una maswali yoyote au shaka kuhusu uhuru wako kama mshiriki wa utafiti, tafadhali wasiliana na Meneja wa NORC IRB kupitia nambari bila malipo ya (866) 309-0542. Bodi ya Marudio ya Taasisi inafanya kazi chini ya sheria za serikali na wanapitia uchunguzi kuhusu watu ili kuhakikisha kuwa washiriki wa utafiti wanawekwa kwa maadilu, usalama na haki.

Do you have any questions about this study? If you have any questions or concerns regarding this study please ask. If you think of them later, contact the study number at 866-315-7130.

Je, una maswali yoyote kuhusu utafiti huu? Iwapo una maswali yoyote au shaka kuhusu utafiti huu, tafadhali uliza. Iwapo utayafikiria baadaye, wasiliana na nambari ya utafiti kwa 866-315-7130.

What if I do not want to be in this study? If you do not wish to participate, we sincerely thank you for your time.

Je, iwapo sitaki kuwa katika utafiti huu? Iwapo hutaki kushiriki, tunakushukuru kwa wakati wako.

If you would like to participate: You must be 18 to 49 years of age to take part in this research study.

Iwapo ungependa kushiriki: Ni lazima uwe kati ya miaka 18 hadi 49 ili kushiriki katika utafiti huu.

Participation in this study implies that you have reviewed and understand what is being asked of you for this study and that you are voluntarily willing to take part of this study. Your answers will be private and you can stop at any time.

Kushiriki katika utafiti huu kunamaanisha kuwa umepitia na kuelewa kinachohitajika katika utafiti huu na kuwa unajitolea kushiriki katika utafiti. Majibu yako yatakuwa ya sir na unaweza kuwacha wakati wowote.

Would you like a copy of this form?

Je, ungependa nakala ya fomu hii?